Mwongozo wa Familia wa Kujifunza

Muhtasari wa yale watoto wanastahili kufahamu na kuweza kufanya na njia za familia kuongeza masomo nyumbani.

“Tunaamini familia ni wenzetu. Niwa kwanza na waelimishaji wa watoto wenye nguvu zaidi . Pamoja tutahakikisha mafanikio ya wanafunzi wote.”

- Mrakibu Emmanuel Caulk,
Shule za umma za kata ya Fayette

Kuhusu mwongozo wetu wa kujifunza:

Muongozo huu unaonyesha baadhi ya vitu muhimu mtoto wako anapaswa kujua na kuweza kufanya kulingana na kiwango cha utayari wa shule. Malengo ya kujifunza inasaidia familia na walimu kujua ni lini wanafunzi wanaweza kuhitaji msaada zaidi na lini wanahitaji changamoto zaidi.

Famila zinaweza kufanya nini?

Kuna mengi unayoweza kufanya kusaidia masomo ya mtoto wako na kusaidia kuwatayarisha kwa maisha yao yajayo. Hapa kuna mambo machache ambayo tatawasaidia wanfunzi kufanikiwa:

1. Waambie masomo ni muhimu, kwamba ndio msingi wa mafanikio.
2. Fanya shule kuwa kipa umbele kwa kumfikisha mtoto wako shuleni bila kuchelewa kila siku.
3. Hudhuria mikutano na matukio mengine ya shule kila mara ikiwezekana.
4. Jishughulishe na shule kujenga kuheshimiana.
5. Himiza kujitegemea; waruhusu watoto kufanya makosa na kisha wakubali wajibu wa chaguo lao.
6. Jadili na mtoto wako kuhusu nini kinafanyika shuleni.
7. Wasiliana mara kwa mara na mwalimu wa mtoto wako kuhakikisha mtoto wako anafaulu mwaka mzima.
8. Una haki ya kujua jinsi mtoto wako anavyendelea; usisite kuwasiliana mwalimu wake kama una maswali.
9. Jenga misamiati ya mtoto wako. Kwa kutumia maoni katika mwongozo huu wa masoma na kuwa na mazungumzo yenye maana na ya kukusudia pamoja na motot wako kila siku, unaweza kujenga misamiati. Kujua maneno mengi na maana ni dalili muhimu ya mafaniko shuleni.

Kuzungumza na Mwalimu wa Utotoni wa Mtoto Wako

Ni muhimu kuwasiliana na mwalimu wa mtoto wako na shule kila mara kuhusu maendeleo ya mwanafunzi na kuhusu maendeleo ya mwanafunzi wako kuhusu. Hapa kuna mifano ya maswali unayoweza kuuliza: mafunzo.

- Mtoto wangu ana nguvu wapi na ni wapi anahitaji kuboresha?
- Maendeleo ya mtoto wangu yanapimwa vipi katika mwaka mzima?
- Naweza kuona mifano ya kazi za mtoto wangu? Vipi wanafikia ama hawafikii malengo ya masomo?
- Mtoto wangu yuko njiani kufikia malengo ya masomo ya darasa lake? Kama sivyo, kuna misaada gani shule inaweza kutoa? Naweza kufanya nini nyumbani?
- Mtoto wangu yuko kwa ama juu ya matarajio ya masomo? Kama ndivyo, nini kingine shule inaweza kutoa? Naweza kufanya nini nyumbani?
- Umesoma IEP ya mtoto wangu? Ni misaada gani inayonayofanyiwa mtoto wangu?
- Mtoto wangu anajifnuza Kiingereza. Kukua kwa lugha ya mtoto wangu kunasaidiwa vipi shuleni?

Kuzungumza na Mtoto wako

Hii inasikika kama kawaida?
“Shule ilikuwaje leo?”
“Sawa”
“Ulifanya nini?”
“Hakuna”
Hiyo ni sawa, endelea kuuliza!

Wanafunzi ambao wazazi wao wanazungumza nao kuhusu shule hufanya vizuri kimasomo katika shule.. Hizi ni baina ya njia za kumhusisha mtoto wako na kusaidia katika mafaniko yao:

- Tenga wakati fulani kila siku kuzungumza na mtotowako kuhusu shule. Uliza mtoto wako ni darasa gani alipendelea zaidi leo. Kwa nini? Ni kitu gani kimoja angeweza kubadilisha kuhusu siku hiyo? Kwa nini?
- Uliza mtoto wako akueleze kitu kimoja walijifunza wamejifunza leo. Ni nini mtoto wako anafikiri inavutia sana? Ni nini inaonekana kuwa ngumu?
- Pitia makaratasi na miradi ambayo mtoto analeta nyumbani kutoka shuleni. Uliza mtoto wako akueleze inaonyesha mafunzo gani?
- Sifia mtoto wako kwa kazi ngumu na juhudi, sio wakati tu “majibu ni sahihi”.
- Uliza maswali kuhusu mtoto wako anawaza nini? Unafikiri nini? Unatambua nini? Uliifanya hivyo kwa nini? Kuna njia nyingine ya kupata jibu hilo?

Kusaidia mafunzo mbali na shule

Masomo hayapaswi kusima wakati wanafunzi wanaacha shule. Hapa kuna baina ya njia unaweza kusaidia masomo nje ya darasa:

- Somea mtoto wako, soma na mtoto wako, na uhimize mda wa familia kusoma pamoja — katika lugha unayoipendelea.
- Tenga wakati mtulivu na mahali starehe kwa mwanafunzi wako kufanya kazi za shule za nyumbani ama shughuli zingine za masomo.
- Hakikisha kuwa wewe na mtoto wako mko na kadi ya maktab na mnajihushisah na shughuli za kusoma kwa familia nzima.
- Jaribu kutengeneza ratiba ya kawaida ya kufanya kazi za shule za nyumbani na shughuli zingine za masomo.
- Tumia muongozo huu kwa malengo machache ya masomo; jaribu mapendekezo kadhaa ya masomo ya nyumbani.

Ni nini mwanafunzi wako anapaswa kujua na kuweza kufanya katika sanaa ya lugha ya kiingereza (ELA):

Kusema na Kusikiliza (mchakato wa mawasiliano)

- Uwezo wa kuzungumza na wenigine pamoja na kueleza hisia na kuuliza maswali katima mazungumzo rahisi.
- Kutumia sentensi rahisi kujieleza.
- Uwezo wa kufuata maagizo rahisi.
- Uwezo wa kumtizama msemi, kusikiza na kuelewa nini kinasemwa.
- Kueleza tena tukio la hivi majuzi ama hadithi ya kwaida na kujadili ni nini kilitendeka.

Kusoma na Fasihi

- Soma maneno ya kawaida nyumbani, mtaani, ama penginepo katika mazingira ya mtoto wako. Kwa mfano: ishara ya kawaida, kama vile KUTOKA, na maneno yanayotumika mara kwa mara, kama vile “the”.
- Soma na kurudia A-B-C.
- Soma kitabu kilichoundwa kwa wasomaji wachanga na tambua kichwa, muandishi, na mtambulishi, kama vile “Bear hudhurungi, bear hudhurungi, Unaona nini?” na Bill Martin Jr. na Eric Carle, ama “Bi Wishy Washy”, na Joy Cowley.
- Tambua mada kuu, wahusika, na matukio katika kitabu ambacho mtoto wako anakisoma ama ambacho wanasomewa.
- Shika kitabu sawa sawa (fahamu mbele na nyuma ya kitabu) na geuza ukurasa.
- Fahamu na uweze kutambua maneno ya alfabeti, haswa maneno katika majina yao.

Kuandika

- Tumia mchanganyiko wa michoro, mazungumzo, na kuandika kupitisha ujumbe kwa wengine.
- Watoto huanza kuandika kwa “kuchorachora” na kisha wanaendelea kuandika herufi na maneno wanavyoendelea kupata uzoefu zaidi wa kuandika baadaye wanaelekea kuandika herufi na majina.
- Chora miundo unapopewa modeli ama mfano.

Jinsi ya Kuhimiza Mafunzo ya ELA Nyumbani:

- Wasiliana na mtoto wako mchano kutwa. Hakikisha unasikiza na kujibu kauli na maswali ya mtoto. Anzisha maneno mapya wakati unaofaa.
- Jibu maswali ya mtoto wako kwa subira hata ikiwa umeshayajibu mara nyingi awali.
- Uliza mtoto wako kuhusu hisia zao. Wape maneno ikiwa hawana misamiati inayohitajika kueleza hisia zao. Mbali na maneno kama “furaha” na “huzuni”, tumia maneno kama “sikitika”, “nafuu”, na “hasira.”
- Uliza mtoto wako maswali kuhusu mazingira yao (“Kwa nini unafikiri hiyo ilifanyika?”) ama (“Unafikiri nini kitatendeka baadaya?”). Aina hii ya maswali inatoa fursa kwa mtoto wako kuongeza mawazo mapya na kurefusha mazungumzo. Maswali kama haya hayana jibu tu moja sahihi kwa hiyo mtoto wako anaweza kuchunguza mawazo yao.
- Toa uzoefu mpya kwa mtoto wako kutizama na kujifunza maneno mapya, kama kufanya safari kwenda kiwanja cha ndege ama kwa sehemu ya makumbusho ya watoto.
- Wacha mtoto wako asaidie na shughuli rahisi. Mtoto wako anaweza kusaidia kuweka midoli katika kikapu, kuweka viatu katika kabati na kusaidia kuweka mataulo katika kabati.
- Unapokuwa unamsomea mtoto wako muulize maswali kuhusu hadithi, picha, na ni nini anafikiri kitafanyika. Zungumza kuhusu matukio kwenye hadithi.. Kama kuna watu, mahali ama matukio katika hadithi ambayo inalingana na uzoefu wako wa kila siku, zungumza kuhusu uhusiano huo. Kwa mfano, unaposoma “Katapila Mwenye Njaa Sana”, zungumza kuhusu hadithi pamoja na wakati ambapo umeona katapila nje ama umekula chakula sawa.
- Himiza mtoto wako akusomee. Ambia mtoto wako atizame picha na kisha kukueleza hadithi.
- Soma mwenyewe. Watoto haswa wanaweza kusoma ikiwa wataona familia na walezi wakisoma magazeti, magazini na vitabu.
- Zungumza na mtoto wako kuhusu herufi za alfabeti lakini ifanye raba! Tumia vitabu vya alfabeti, puzzles au herufi katika jina la mtoto. Zungumza kuhusu herufi unazoziona katika mazingira – kwa ishara, vitabu, na waraka unaoandika.
- Furahia mufanya mashairi na mtoto wako. Imba nyimbo za mashairi na soma vitabu vya mashairi pamoja.
- Mhimize mtoto wako kuandika. Mpe aina tofauti ya mahitaji ya shule kufanya kuandika kuvutie, aina tofauti ya makaratasi, marker, penseli na kreyon. Usijali kama mtoto wako haandiki herufi zote sawa. Hiyo kuchorachora ni mazoezi mazuri kwa maandishi yote atakayofanya baadaye shuleni.
- Uliza mtoto wako akueleze kuhusu maandishi yao. Mara nyingi watoto watakueleza walitaka kusema nini kisha unaweza kuandika neno walilolisema kando ya maandishi yao.
- Mpe mtoto wako jambo lakuandika kuhusu. Kutengeneza kadi ya siku ya kuzaliwa ya bibi ama kuandika waraka kwa mwalimu ni mambo uzoefu wa maana.
- Himiza na pongeza mtoto wako kwa juhudi zao za kuandika. Hakikisha kuonyesha kazi zao.
- Toa maoni kuhusu maandishi na chapa unazoziona nyumbani mwako kwa maboksi ya nafaka, resepi na kwa kompyuta. Onyehsa na kusoma maandishi haya kwa mtoto wako unapoendelea na shughuli zako mchana kutwa.
- Himiza mtoto wako kuandika jina lao. Saidia na herufi inavyotakikana, na unaweza pia kuandika.

Tafadhali ungana na mwalimu wa mtoto wako na uulize kuhusu rasilimali za masomo ya watoto wa preskuli na familia ambazo zinahusiana na ujuzi wa ELA.

Ni nini mwanafunzi wako anapaswa kujua na kufanya katika Hesabu:

- Hesabu angalau hadi 10 na hadi 30.
- Tofautisha na uandike nambabri hadi 20.
- Tambua nambari zilizoandikwa.
- Tambua, Eleza, panua, na tengeneza chati ama michoro rahisi. Kwa Identify, describe, extend, and create simple patterns Kwa mfano: ABABABA ama nyekundu, bluu, nyekundu, blee, nyekundu, bluu, nyekundu, bluu.
- Tambua na ueleze miundo yenye pande mbili kulingana na sifa zake. Kwa mfano: mraba una kona ama pembe nne.
- Tambua na umezhi viwango vidogo kwa maneno ya nambari kama “moja”, “mbili”, “tatu”.
- Tumia ukubwa wa maneno kama vile “mingi”.
- Tumia maneno kama “sawa na” kulinganisha.
- Tambua ama panga vitu katika vikundi vidogo (kama kwa rangi na saizi).
- Elewa utaratibu wa siku kama vile “asubuhi” na “usiku”.

Jinsi ya Kuhimiza Mafunzo ya Hesabu Nyumbani:

- Hesabu na mtoto wako katika shughuli za kila siku. Hesabu nambari za taulo zitakazokunjwa ama nambari ya kuki unahitaji kwa rafiki zako.
- Wakati ungali unacheza na mtoto wako, peana nafasi yake kutofautisha. Kwa mfano, uliza mtoto wako ni nani ana makaratasi mengi ama ni nani ana maji ya matunda kidogo.
- Onyesha nambari katika mazingira yako na zungumza kuhusu jinsi zinavyotumika. Hii ni pamoja na ishara za viwango vya mbio za magari, saa, na bei katika menyu ama kwa vitu katika soko ama dukani.
- Zungumza kuhusu miundo na mtoto wako. Tilia makini miundo unayoiona katika makazi yenu (mlango ni rektango na dirisha ni mraba). Miundo ya vitabu inaweza pia kuwa raha!
- Unapozungumza na mtoto wako, tumia maneno kuelezea mahali vitu vilipo kama “chini”, na “zaidi ama juu” pia na maneno yanayohusu muda kama siku za wiki, jana, ama kesho.
- Cheza michezo ya kulinganisha na mtoto wako. Michezio kama “kumbukumbu” saidia mtoto wako kukuza ujuzi wake wa kulinganisha.
- Himiza mtoto wako kuelezea vitu ama kuvigawanya. Kwa mfano, kuchagua mapeni na nickels katika vikundi tofauti ama kuchagua gari za bluu na nyekundu katika michezo tofauti ya gereji.
- Patia mtoto wako nafasi ya kuchunguza kupima – kwa kutumia vikombe vya kupima na mizani inaweza kuwa uzoefu wa raha ya mafunzo. Pia wacha mtoto wako “apima” vitu katika njia ya raha. Kwa mfano, “kitanda chako kina urefu wa viatu vingapi?” ama “inachukua hatua ngapi kufikia jikoni?” Hesabu na mtoto wako katika shughuli za kila siku. Hesabu nambari ya taulo za kukunjwa ama nambari ya kuki ambazo unahitaji kwa rafiki zako.
- Wacha mtoto wako asaidie na shughuli za nyumbani kama vile kuandaa meza. Hii inakuza kuhesabu na kuwasiliana moja-kwa-moja napkini moja kwa kila sahani.

Tafadhali ungana na mwalimu wa mtoto wako na uulize kuhusu rasilimali za masoma ya nyumbani kwa watoto wa preskuli na familia ambazo zinahusiana na ujuzi wa hesabu.

Ni nini mwanafunzi wako anapaswa kujua na kufanya katika sanaa masomo ya sanaa

- Hudhuria na onyesha hamu katika baadhi ya sanaa, densi, muziki, na uzoefu wa michezo wa kuigiza.
- Nyumbani, mpe mtoto wako fursa nyingi ambazo ni pamoja na kupaka rangi, kukanda unga, na kuchora. Mpe mtoto wako vitu tofauti vya sanaa (markers, rangi, gluu, karatasi, na kadhalika) na nafasi ya kufanya sanaa yenye kusababisha “uchafu”.

Elimu ya Afya

- Onyesha afya ya akili katika watu binafsi na mazingira ya muungano wa jamii. Mfano ni pamoja na kuweza kuosha mikono kwa kujitegemea na kula chakula chenye afya; kucheza pamoja na watoto wengine.
- Nyumbani, saidia mtoto wako kuosha mikono na kusugua meno kama inavyohitajika. Zungumkza na mtoto wako kuhusu marafiki zao na inamaanisha nini kucheza pamoja kwa kushirikiana. Cheza pamoja na mtoto wako. Himiza mtoto wako awe msaidifu na asaidie wengine.

Elimu ya kimwili na ujuzi wa /Misuli (mikubwa) na Misuli (midogo)

- Onyesha ujuzi wa kulingana ambao unamsaidia mtoto wako kukimbia, kuruka, na kuruka kamba.
- Onyesha ukitumia mikono na vidole kufunga vifungo, kushika, kufunga zipu, ama kuandika.
- Nyumbani, peana nafasi kila siku ya mtoto wako kucheza nje (na vifaa tofauti ambazo ni pamoja na baiskeli/traiskeli, na michezo kama hopskoch ambayo inahimiza kuruka kamba na kuruka) na kufanya shughuli kama vile kukanda unga wa ngano, legos, na makasi na karatasi.

Sayansi

- Onyesha njia tofauti za kisayansi za kuwaza na kufanya kazi ambazo zinaonyesha kuelewa ulimwengu unaowazunguka, himiza ujuzi wa kutatua matatizo, na saidia na udadisi wa jinsi vitu vinavyofanya kazi.
- Nyumbani, tembelea shambani, dukani, ama nenda ukatembee na mtoto wako na zungumza kuhusu uzoefu. Uliza mtoto wako jinsi vitu vinaonja, kunukia, na kusikika wakati vikiguswa. Fanya utafiti wa majibu kwa mtoto maswali ya mtoto wako ya jinsi vitu vinafanya kazi “Ngurumo ni nini?”) kwa kufanya uchunguzi wa majibu pamoja ukitumia kamusi, mtandao, ama vitabu.

Masomo ya Kijamii

- Onyesha msingi wa kuielewa dunia kwa kutambua familia, marafiki, na wageni.
- Onyesha kuelewa kwako kwamba watu wanatoka sehemu mbalimbali.
- Onyesha uwezo wa kufuata masharti rahisi.
- Nyumbani, weka kiwango chenye busara kwa mtoto wako na saidia mtoto wako kufuata viwango hivyo. Saidia mtoto wako kuelewa kwamba masharti tofauti yanapeanwa katika makao tofauti. Kwa mfano, kutumia sauti ya chini katika maktaba. Kuwa na mazungumzo na mtoto wako kuhusu familia yako. Chora picha kuonyesha wanajamii. Tumia nafasi za kila siku kuzungumza kuhusu jinsi watu walivyo sawa ama tofauti.

Tafadhali ungana na mwalimu wa mtoto wako na uulize kuhusu rasilimali za masoma ya nyumbani kwa watoto wa preskuli na familia ambazo zinahusiana na ujuzi wa uliopo hapo juu.

FAYETTE COUNTY PUBLIC SCHOOLS
1126 Russell Cave Road
Lexington, KY 40505

859-381-4100
www.fcps.net

Brosha hii imechapishwa na shule za umma za kata ya fayette.

Ilitengenezwa Fall 2016